GRADE 6 END OF YEAR EXAMS

MTAALA WA UMILISI

KISWAHILI – GREDI YA 6

Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali yanayofuata.

Hapo zamani za kale, katika ulimwengu wa wanyama, paliishi Swara na **Mbweha Swara na Mbweha walipendana kama chanda na pete.** Wawili hao walikuwa na familia zao. Kila mmoja alikuwa na nyumba yake, mke pamoja na watoto. Mbweha alikuwa na watoto sita naye Swara alikuwa na watoto watano. Marafiki hao **walifanya mambo yao kwa ushirikiano mkubwa**. Walifuga wanyama kama vile mbuzi, ng'ombe, kondoo na ngamia. Wanyama hao waliwapa faida ya maziwa na wakati fulani kuwafanyia kazi.

Tofauti kubwa iliyokuwapo ni kuwa Swara alipenda shughuli za kilimo naye Mbweha alipenda sana ufugaji. Swara alipouza maziwa yake, alipanda miche kisha akaamua kuwekeza katika kilimobiashara. Alipanda mimea kama vile michungwa, mihindi, mitufaha na mingine. Alipovuna mazao ya mimea hiyo, alitoa gharama ya ukulima huo kisha akabaki na faida kubwa mno. Kwa kuwa kazi ilikuwa nyingi shambani, aliamua kuwapa wanyama wengine ajira. Kila alipovuna mazao yake, aliyauza na kuweka pesa alizozipata katika benki. Hiyo ilikuwa njia ya kuhakikisha kuwa pesa zake zisingeibwa na wahalifu. Uzalendo wa Swara ulijulikana sana alipolipa ushuru kutokana na mapato.

Kwa sasa, marafiki hao wawili ni matajiri wakubwa. Wakazi katika eneo hilo wanapenda sana kilimo, ufugaji na biashara. Vilevile, wao hulipa ushuru wa mapato mara kwa mara. Wamejifunza kwa Swara na Mbweha kuwa kulipa ushuru kuna manufaa makubwa katika nchi.

1. Ukirejelea maisha ya Swara, ni jambo gani lililokuwa la mwisho kati ya mambo haya?
    A. kulipa ushuru
    B. kuuza mazao ya shambani
    C. kufuga wanyama
    D. kuanzisha kilimo
2. Maneno **'walifanya mambo yao kwa ushirikiano mkubwa'** yanaonyesha kuwa Swara na rafiki yake walizingatia methali gani?
    A. Achanikaye kwenye mpini hafi njaa.
    B. Majuto ni mjukuu huja baadaye.
    C. Mkono mmoja hauchinji ng'ombe.
    D. Panya wengi hawachimbi shimo.
3. Ni kweli kuwa kama Swara asingekuwa na mifugo;
    A. angekosa wanyama wa kumfanyia kazi shambani.
    B. angekosa pesa za kuweka katika benki.